**HOTUBA YA MHE CHARLES MAKONGORO NYERERE, MKUU WA MKOA WA RUKWA KWENYE SEMINA YA UDHIBITI WA KELELE KWA WAMILIKI WA KUMBI ZA STAREHE, STUDIO NA MAENEO YA KUABUDIA/MAKANISA TAREHE 27 JUNI, 2023**

- ***Katibu Tawala Mkoa,***
- ***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,***
- ***Viongozi wa dini,***
- ***Wataalam wa Mkoa na Halmashauri za Wilaya,***
- ***Wamiliki wa Kumbi za Mikutano,***
- ***Wamiliki wa Studio,***
- ***Wafanyabiashara,***
- ***Waandishi wa Habari.***

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…………….**

Awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na Baraka kwa kuweza kutukutanisha hapa tukiwa wazima na wenye afya njema, pili namshukuru sana Meneja wa Kanda Magharibi wa NEMC kwa kukubali wito wa kuja hapa kuungana nasi katika tukio hili muhimu la kuwapa elimu wamiliki wa kumbi za starehe, studio na viongozi wa dini kuhusu uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na kelele.

***Ndugu Washiriki,*** Hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la uchafuzi wa mazingira unaotokana na kelele na mitetemo inayotokana na shughuli za kiuchumi zinazoendeshwa katika maeneo ya Bar, Kumbi za starehe na maeneo ya kuabudia yaliyopo katika makazi yetu. Kufuatia changamoto hizi, NEMC ilianza kuchukua hatua katika maeneo mbalimbali kwa kuzingatia sheria ya usimamizi wa mazingira sura Na. 191, kanuni na miongozo ya mwaka 2015.

***Ndugu Washiriki,*** Kupitia hatua hizo ambazo NEMC walianza kuzichukua kuhusu uchafuzi wa Mazingira unaosababishwa na kelele**,** Mhe. Waziri Mkuu alituelekeza Wakuu wa Mikoa yote Nchini kukaa pamoja na Mabaraza ya Biashara, Wamiliki wa kumbi za starehe waliopo katika maeneo yetu ya kiutawala ili kutafuta muafaka wa

pamoja katika utekelezaji wa Sheria, Kanuni na miongozo kuhusu udhibiti wa athari zitokanazo na sauti zilizozidi viwango.

***Ndugu Washiriki,*** Najua kila mmoja anao uhuru wa kujitafutia riziki, ingawa katika utafutaji wa riziki lazima sheria za nchi zizingatiwe ikiwemo kutoa nafasi kwa kila mtu kufanya shughuli za uzalishaji mali bila kumuathiri jirani yake. Idara za mipango miji zihakikishe zinasimamia miongozo inayoelekezwa na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kuhakikisha kuwa inapanga miji kwa kuzingatia matumizi . Mfano maeneo ya makazi, viwanda, maeneo ya ibada na maeneo ya huduma za jamii kama shule, hospitali michezo n.k.

***Ndugu Washiriki,*** Shughuli za kijamii zizingatie mwongozo wa udhibiti wa uchafuzi wa mazingira unaotokana na kelele na mitetemo kwa kuhakikisha kuwa utoaji wa leseni na vibali unazingatia mwenendo na maelekezo yaliyotolewa kwa matumizi ya vibali hivyo. Katika Mkoa wa Rukwa tatizo la kelele sio kubwa sana ingawa hatuna budi kuanza kuelimishana kutokana na ukuaji wa miji yetu ya Sumbawanga, Matai na Laela na Namanyere.

***Ndugu Washiriki,*** Sauti zinazozidi viwango zinaathari kwa afya za wakaazi wa maeneo ya jirani zinakotoka sauti hizo ikiwemo tatizo la kusikia vizuri, kukosa usingizi na kusababisha migogoro kati ya wakazi na wazalishaji wa kelele hizo. Aidha, kelele zikizidi zinaathiri utendaji wa kazi kutokana na watu kukosa usingizi mzuri unaopelekea jamii inayozunguka maeneo hayo kutopata usingizi mzuri.

***Ndugu Washiriki,*** Napenda kuwakumbusha wamiliki wa maeneo ya burudani, starehe na nyumba za ibada, wamiliki wa studio kuzingatia matumizi ya vipima kelele ili kuzuia sauti inayozidi yenye athari kwa jamii inayozunguka maeneo hayo. Sheria ya Mazingira Sura ya 191, Kifungu cha 106 (5 na 6) kinazuia kutoa kelele inayozidi viwango vilivyoruhusiwa. Shirika la Afya Duniani (WHO) limebainisha kelele kuwa ni mojawapo ya vitu hatarishi katika maisha ya binadamu. Kwa mujibu wa *“European Environmental Agency” (EEA, 2018)* kelele ni kisababishi cha vifo vya mapema kwa watoto *“Pre-mature death”.* Hivyo, uchafuzi wa maazingira

unaosababishwa na kelele na mitetemo ni miongoni mwa kero kubwa inayohatarisha afya kwa jamii.

***Ndugu Washiriki;*** Mwaka 2021 Serikali iliandaa mwongozo wa udhibiti wa uchafuzi wa mazingira utokanao na kelele na mitetemo, mwongozo huu ulizielekeza **Mamlaka za Serikali za Mitaa** kuhakikisha zinatekeleza majukumu yao yaliyoainishwa kwenye **mwongozo huo kwa kuchukua hatua kudhibiti kelele zilizozidi viwango** ikiwa ni pamoja na kutozwa faini na kufungiwa biashara kwenye maeneo yaliyokithiri kwa kelele na mitetemo kwani wanaoathirika zaidi ni watoto na wazee. Madhara mengine yanayosababishwa na kelele zilizokithiri ni pamoja na kuzuka kwa migogoro, kupelekea vifo, kupata ukiziwi, msongo wa mawazo kutokana na kukosa utulivu, kutokulala, kuongezeka kwa mapigo ya moyo na kupelekea shinikizo la damu, hivyo hizi kanuni zimewekwa ili kulinda afya za binadamu.

***Ndugu Washiriki,*** mwisho niwashukuru sana wote kwa  kufika kwenye kikao hiki, ni matumaini yangu kuwa mtaendelea kutoa ushirikiano kwa wataalam, jamii zinazozunguka maeneo yetu na taasisi nyingine za serikali zinazosimamia kanuni na miongozo wakiwemo baraza la usimamizi wa mazingira NEMC ili kuhakikisha jamii inabaki kuwa salama na yenye afya kupitia uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na kelele na mitetemo.

Mungu Ibariki Tanzania,
Mungu Bariki Mkoa wetu wa Rukwa,
Asanteni sana kwa kunisikiliza

Charles Makongoro Nyerere

**MKUU WA MKOA WA RUKWA**